# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS

## TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**MAELEKEZO MAHSUSI KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU NA KAMATI ZA UCHUNGUZI KUHUSU NAMNA YA KUENDESHA UCHUNGUZI WA MASHAURI YA NIDHAMU TOLEO NA. 2 LA MWAKA 2024**

***Imetolewa Na:***

Tume ya Utumishi wa Umma,
Jengo la Chiwanga (UDOM),
Ghorofa ya 2,
2 Barabara ya UDOM,
S.L.P. 1074,
**40405 DODOMA**.

**DESEMBA, 2024**

**DIBAJI**

Maelekezo haya mafupi ni mahsusi kwa Mamlaka za Nidhamu na Kamati za Uchunguzi kuhusu namna ya kuendesha uchunguzi wa mashauri ya nidhamu katika Utumishi wa Umma.

Lengo la maelekezo haya ni kuzisaidia Mamlaka za Nidhamu na watumiaji wengine kuunda Kamati za Uchunguzi kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Aidha, maelezo haya yataziwezesha Kamati za Uchunguzi kujua wajibu wake na kuzirahisishia utekelezaji wa majukumu yake.



Mathew M. Kirama
**KATIBU**
**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**MAELEKEZO MAHSUSI KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU NA KAMATI ZA UCHUNGUZI KUHUSU NAMNA YA KUUNDA NA KUENDESHA UCHUNGUZI WA MASHAURI YA NIDHAMU**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.1** Kwa mujibu wa Kifungu cha 23(2)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 [Marejeo ya Mwaka 2019] na Kanuni ya 45 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, Mamlaka ya Nidhamu ina wajibu wa kuunda Kamati ya Uchunguzi pale inapothibitika kwamba mtumishi mtuhumiwa:

(i) Katika utetezi wake amekana mashtaka;

(ii) Katika utetezi wake amekiri makosa na kutoa sababu za kutenda makosa hayo;

(iii) Utetezi wake haujitosherezi; na

(iv) Hakujitetea kabisa.

**1.2 Kamati ya Uchunguzi ni nini?**

Kamati ya Uchunguzi ni chombo kinachotumiwa na Mamlaka ya Nidhamu pale inapohitaji kupata uthibitisho wa kutendeka au kutokutendeka kwa tuhuma zinazomkabili mtumishi ili Mamlaka husika iweze kutoa uamuzi sahihi wa mashauri ya nidhamu yanayowakabili watumishi wake.

## 2.0 WAJIBU WA MAMLAKA YA NIDHAMU

### 2.1 Ni mamlaka ya Uteuzi

(i) Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 [Marejeo ya Mwaka 2019] na Kanuni 45(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, mamlaka ya uteuzi wa Kamati ya Uchunguzi ni Mamlaka ya Nidhamu husika.

(ii) Mamlaka ya Nidhamu ina wajibu wa kumtaarifu mtumishi mtuhumiwa kuhusu kuundwa kwa Kamati ya Uchunguzi dhidi yake.

### 2.2 Hadidu za Rejea

(i) Mamlaka ya Nidhamu ina wajibu wa kutoa hadidu za rejea kwa Kamati ya Uchunguzi.

(ii) Hadidu za rejea zitakabidhiwa kwa Kamati ya Uchunguzi kabla ya uchunguzi kuanza.

### 2.3 Maudhui ya Hadidu za Rejea

Hadidu za Rejea ni maelekezo maalum ya Mamlaka ya Nidhamu kwa Kamati ya Uchunguzi. Hadidu hizo zitazingatia:-

(i) Hati ya mashtaka na Kanuni zilizokiukwa;

(ii) Muda wa kuendesha na kuwasilisha Taarifa ya Uchunguzi; na

(iii) Kuhakikisha kuwa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo vinazingatiwa wakati wa kutekeleza majukumu yake.

### 2.4 Muundo na Sifa za Kamati ya Uchunguzi

(i) Mwenyekiti na Wajumbe wawe ni watumishi wa Umma;

(ii) Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi lazima wawe na cheo cha Uandamizi na kuendelea;

(iii) Wajumbe wawe na cheo kinacholingana na cha mtumishi mtuhumiwa au zaidi;

(iv) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi atoke Taasisi nyingine;

(v) Kamati ya Uchunguzi iwe na Wajumbe si chini ya wawili(2) na si zaidi ya wanne (4);

(vi) Uteuzi wa Wajumbe uzingatie Jinsi;

(vii) Mamlaka ya Nidhamu isiwe mjumbe mmojawapo wa Kamati ya Uchunguzi; na

(viii) Kamati ya Uchunguzi pale inapochunguza suala la kitaalamu na ikaona kuna umuhimu wa kupata mtaalamu ambaye anaweza kuisaidia, Kamati inaweza kuiomba Mamlaka ya Nidhamu kupewa wataalam wasiozidi wawili (2) wenye taaluma na ujuzi wa jambo linalochunguzwa.

### 2.5 Muda wa Uchunguzi

(i) Kamati ya Uchunguzi lazima iundwe ndani ya siku sitini (60) kuanzia tarehe ya kutolewa kwa Hati ya Mashtaka;

(ii) Muda wa uchunguzi usizidi siku sitini (60) kuanzia tarehe ya kuanza uchunguzi;

(iii) Iwapo uchunguzi hautakamilika ndani ya muda wa siku sitini (60), kibali cha kuongeza muda kitaombwa kwa Mamlaka ya Nidhamu na Mamlaka ya Nidhamu itatoa muda wa nyongeza usiozidi siku thelathini (30); na

(iv) Iwapo uchunguzi utakuwa haujakamilika baada ya siku thelathini (30) za nyongeza kutolewa na Mamlaka ya Nidhamu, kibali cha kuongeza muda kitaombwa na Mamlaka ya Nidhamu kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) ambaye naye ataongeza muda usiozidi siku thelathini (30). Aidha, nyongeza hii ndiyo ya mwisho kwa mujibu wa Kanuni.

## 3.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA NA MAMLAKA YA NIDHAMU WAKATI WA KUUNDA KAMATI NA KUFANYA UCHUNGUZI

Kwa mujibu wa Kifungu cha 23(2)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 [Marejeo ya Mwaka 2019], Kanuni ya 45 hadi 49 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na Nyaraka mbalimbali, mambo muhimu ya kuzingatiwa na

Mamlaka ya Nidhamu wakati wa kuunda Kamati ya Uchunguzi na wakati wa kufanya uchunguzi wa mashauri ya nidhamu ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha kuwa uteuzi wa Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi umezingatia matakwa ya Kanuni ya 46 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022;

(ii) Kutoa hadidu za rejea kwa Kamati ya Uchunguzi kuhusu tuhuma zinazowakabili watumishi watuhumiwa;

(iii) Kuipatia Kamati ya Uchunguzi Nyaraka zote zinazohusu Shauri la Nidhamu dhidi ya watumishi watuhumiwa;

(iv) Kuipatia Kamati ya Uchunguzi mtu mwenye utaalamu au uzoefu kuhusu shauri linalochunguzwa;

(v) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Uchunguzi imemjulisha mtumishi mtuhumiwa na mashahidi kuhusu siku, tarehe, muda na mahali ambapo kitafanyika kikao cha uchunguzi angalao siku saba (7) kabla ya mahojiano na Kamati;

(vi) Kuhakikisha kuwa mtumishi mtuhumiwa amepewa haki ya kuwepo wakati wa uchunguzi, kusikilizwa kwa ukamilifu, kuhoji mashahidi wa Mamlaka ya Nidhamu, kuona vielelezo vya mamlaka ya Nidhamu na kuwasilisha vielelezo vyake;

(vii) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Uchunguzi inamruhusu mtumishi mtuhumiwa kuwakilishwa na Mtumishi wa Umma, Wakili au Mwakilishi kutoka Chama cha Wafanyakazi husika;

(viii) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Uchunguzi inamruhusu Mamlaka ya Nidhamu au Mwakilishi wake kufika mbele ya Kamati ya Uchunguzi

(ix) Kuhakikisha kuwa mtumishi mtuhumiwa au Mwakilishi wake anakuwa na haki ya kupewa na kuchunguza nakala ya nyaraka zilizotumiwa na Mamlaka ya Nidhamu kama ushahidi dhidi yake;

(x) Kuhakikisha kuwa mtumishi mtuhumiwa anapewa haki ya kuleta mashahidi wake au kutoa nyaraka muhimu kuhusu shauri linalomkabili;

(xi) Kuhakikisha kuwa uchunguzi unaendeshwa kwa faragha;

(xii) Iwapo kutokana na ushahidi uliotolewa wakati wa uchunguzi, kuna tuhuma mpya zitaibuliwa, Kamati ya Uchunguzi itaijulisha Mamlaka ya Nidhamu ili iweze kumpa mtumishi mtuhumiwa Hati ya Mashtaka ya nyongeza ambayo ataijibu ndani ya siku 14;

(xiii) Iwapo Hati ya Mashtaka yenye tuhuma mpya imetolewa kwa mtumishi mtuhumiwa, Kamati itaendelea na uchunguzi wa tuhuma hiyo na inaweza kuwaita tena mashahidi kwa mahojiano ya ziada;

(xiv) Kuhakikisha kuwa maswali, majibu, na maelezo ya mwenendo mzima wa uchunguzi, pamoja na maelezo ya watu wote waliohojiwa kwa maana ya mtumishi mtuhumiwa, mashahidi wa mtumishi mtuhumiwa, Mamlaka ya Nidhamu na Mashahidi wa Mamlaka ya Nidhamu yanaandikwa kwa ufasaha na kwa ukamilifu kwa ajili ya kumbukumbu;

(xv) Kuhakikisha kuwa Mwenendo na Taarifa ya Uchunguzi vinawasilishwa kwa Mamlaka ya Nidhamu ndani ya muda uliotolewa kisheria;

(xvi) Kuhakikisha kuwa Taarifa ya Uchunguzi inajumuisha maoni kuhusu kuthibitika au kutothibitika kwa tuhuma na sababu za maoni hayo.

(xvii) Kuhakikisha kuwa Kamati ya Uchunguzi inapendekeza aina ya adhabu anayostahili kupewa mtumishi mtuhumiwa na Mamlaka ya Nidhamu; na

(xviii) Mtumishi mtuhumiwa anaweza kupewa nakala ya Mwenendo wa Uchunguzi iwapo ataomba.

## 4.0 WAJIBU WA KAMATI YA UCHUNGUZI

(i) Kupitia hadidu za rejea zilizotolewa na Mamlaka ya Nidhamu na kuandaa utaratibu wa kufanya uchunguzi;

(ii) Kupitia vielelezo vyote vinavyohusu shauri husika;

(iii) Iwapo wakati wa uchunguzi kutajitokeza tuhuma mpya, Kamati ya Uchunguzi itaitaarifu Mamlaka ya Nidhamu ambapo Mamlaka ya Nidhamu itaandaa Hati ya Mashtaka ya Nyongeza na kumpa mtumishi

Mtuhumiwa ambaye atapaswa kuijibu ndani ya siku 14 tangu tangu tarehe ya kuipokea Hati hii;

(iv) Kumtaarifu mtumishi mtuhumiwa, Mamlaka ya Nidhamu na mashahidi wa pande zote siku, tarehe, muda na mahali ambapo kikao cha uchunguzi kitafanyika;

(v) Kumhoji mtumishi mtuhumiwa, Mamlaka ya Nidhamu, Mashahidi au Wawakilishi wa pande zote;

(vi) Kumpa mtumishi mtuhumiwa nafasi ya kujitetea kikamilifu mbele ya Kamati na mashahidi wa Mamlaka ya Nidhamu;

(vii) Kuhakikisha kuwa maelezo ya mtumishi mtuhumiwa, Mamlaka ya Nidhamu na mashahidi wao yanawekwa kwenye maandishi;

(viii) Kutafuta taarifa za ziada kuhusu tuhuma endapo zitahitajika;

(ix) Kutembelea maeneo yanayohusika na tuhuma endapo italazimu;

(x) Kuomba kupatiwa wataalamu wa maeneo yanayochunguzwa endapo italazimu;

(xi) Kuandaa Mwenendo na Taarifa ya Uchunguzi wa shauri la nidhamu;

(xii) Kamati ya Uchunguzi kwenye Taarifa ya Uchunguzi, itamke kama, kwa maoni ya Kamati ya Uchunguzi, tuhuma dhidi ya mtumishi mtuhumiwa zimethibitishwa au la na kutoa sababu za maoni hayo;

(xiii) Kupendekeza aina ya adhabu inayostahili kutolewa dhidi ya mtumishi mtuhumiwa kulingana na matokeo ya uchunguzi; na

(xiv) Kukabidhi Mwenendo na Taarifa ya Uchunguzi kwa Mamlaka ya Nidhamu kwa wakati uliopangwa.

**KIAMBATISHO A**

Nyaraka muhimu zitakazotumika katika kufanya uchunguzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

(ii) Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma Toleo la 2 la mwaka 2008;

(iii) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 [Marejeo ya Mwaka 2019];

(iv) Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022;

(v) Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za Mwaka 2003;

(vi) Mwongozo wa Tume ya Utumishi wa Umma kuhusu Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko kwa Watumishi wa Umma, Toleo Na. 3 la Mwaka 2024;

(vii) Miundo ya Maendeleo ya Utumishi wa Umma (Schemes of Service);

(viii) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma (Standing Orders) za mwaka 2009;

(ix) Kanuni za Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma za mwaka 2023;

(x) Nyaraka mbalimbali kuhusu masuala ya Utumishi wa Umma zinazotolewa mara kwa mara (Establishment Circulars); na

(xi) Maadili ya kitaaluma kulingana na taaluma mbalimbali katika Utumishi wa Umma.